# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

**HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUCHUNGUZA NA KUDHIBITI HESABU ZA SERIKALI (PAC) KUHUSU UWASILISHWAJI WA RIPOTI ZA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2022.**

---

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, Bwana wa viumbe vyote, Muumba Mbingu na Ardhi pamoja na vilivyomo ndani yake, ambae ametujaalia uhai, afya njema na taufiki ya kukutana hapa leo, kwa lengo la kutekeleza majukumu yetu ya kuwatumikia wananchi.

**Mheshimiwa Spika** naomba nikushukuru wewe Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu ili niweze kuzungumzia machache na ya muhimu, yanayohusu uwasilishwaji wa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kipindi cha mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2022 kama ambavyo Kanuni ya 43(1) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2020 inavyoelekeza.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii pia kumshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Mwalimu Haroun Ali Suleiman kwa kuweza kuwasilisha hapa Barazani Ripoti hizi ambazo ndio zitakazotumiwa na Kamati zinazofuatilia na kuchunguza mapato na matumizi ya fedha za umma.

**Mheshimiwa Spika**, pia, napenda kutoa pongezi na shukurani za dhati kwa Wajumbe na Makatibu wa Kamati hii kwa umoja, na ari kubwa waliyonayo wakati wote wa utekelezaji wa kazi za Kamati ikiwa ni pamoja na kazi hii ya kuzipitia na kuzichambua Ripoti za Ukaguzi zilizowasilishwa hapa Barazani.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na umuhimu wao, naomba kuwatambua kwa majina yao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Juma Ali Khatib - Mwenyekiti.
2. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - M/Mwenyekiti.
3. Mhe. Mihayo Juma N'hunga - Mjumbe
4. Mhe. Maryam Thani Juma - Mjumbe
5. Mhe. Sulubu Kidongo Amour - Mjumbe
6. Mhe. Suleiman Haroub Suleiman - Mjumbe
7. Ndg. Maryam Haji Ali - Katibu
8. Ndg. Said Khamis Ramadhan - Katibu

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya PAC inatambua na kuthamini kazi kubwa inayofanywa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, katika kujenga nidhamu ya matumizi ya rasimali za Umma katika Serikali na kuimarisha misingi ya Demokrasia na Utawala Bora hapa nchini hasa ikizingatiwa kuwa Sheria za Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Namba 11 ya mwaka 2016 pamoja na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Namba 12 ya mwaka 2016 zinaelekeza utaratibu na nidhamu ya matumizi yanayofanywa na Wizara na Taasisi za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mnasaba huo, Kamati yangu ina kila sababu ya kuwapongeza kwa dhati Viongozi na Watendaji wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa utekelezaji wa kazi ngumu ya ukaguzi na hatimae kumudu kuandaa Ripoti hizi kama ambavyo kifungu cha 112 cha Katiba yetu kinavyoelekeza.

**Mheshimiwa Spika,** kwa vile ukaguzi ni dhana pana inayohitaji kutekelezwa kwa utaalamu wa hali ya juu, hivyo, Ofisi ya Baraza la Wawakilishi pamoja na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali waendelee kuzipatia mafunzo ya mara kwa mara Kamati hizi zinazosimamia masuala ya Kifedha yakiwemo mafunzo ya utambuzi wa mbinu mpya na aina mbali mbali za Ukaguzi ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati zetu.

**Mheshimiwa Spika,** kati ya Ripoti Saba zilizowasilishwa hapa Barazani, Kamati yetu itahusika na Ripoti Nne za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali zinazohusiana na:

1. Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha Ulioishia tarehe 30 Juni, 2022;
2. Ukaguzi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo (CDF) na Miradi ya maendeleo ya Wadi kwa mwaka wa Fedha 2021/2022;
3. Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Serikali Kuu kwa kipindi cha mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2022; na
4. Ripoti ya Kitaalamu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusiana na Ukaguzi wa Ujenzi na Matengenezo ya Majengo ya Skuli - Unguja na Pemba.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali imezipokea ripoti zote hizo na kuahidi kuzifanyia kazi na kuwasilisha kwa kina taarifa yake mbele ya Baraza hili Tukufu ili Waheshimiwa Wajumbe mupate nafasi ya kuichangia, kutoa mapendekezo na hatimae Serikali kuchukua hatua stahiki kwa wale wote waliohusika na ubadhirifu na upotevu wa fedha za umma.

**Mheshimiwa Spika,** mambo ya jumla ambayo Kamati imeyabaini kupitia Ripoti zilizowasilishwa ni:

**(A) UWASILISHWAJI WA RIPOTI KWA LUGHA YA KIINGEREZA**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa kifungu cha 87 kifungu kidogo cha (1) cha Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984 kinaeleza kwamba lugha rasmi ya Baraza la Wawakilishi itakuwa Kiswahili. Sambamba na hilo, Kanuni ya 25 ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2020, imeelekeza kwamba majadiliano na shughuli za Baraza yataendeshwa kwa lugha ya Kiswahili.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya PAC imepokea Ripoti ya Kitaalamu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusiana na Ukaguzi wa Ujenzi na Matengenezo ya Majengo ya Skuli - Unguja na Pemba ambayo imewasilishwa hapa Barazani kwa lugha ya Kiingereza jambo ambalo linaenda kinyume na Katiba na Kanuni za Kudumu za Baraza letu. Hata hivyo, kwa uzoefu uliopo wa muda mrefu, Afisi ya CAG imekuwa na desturi ya kuwasilisha Barazani Ripoti hizi kwa lugha ya Kiswahili.

**Mheshimiwa Spika,** kwa masikitiko makubwa Kamati ya PAC imejiuliza maswali kadhaa ambayo majibu yake imekuwa kitendawili kisichokuwa na

jibu, kwamba kwanini mara hii Afisi ya CAG imefanya maamuzi ya kuwasilisha Ripoti kwa lugha ya Kiingereza, Jee Afisi ya CAG haioni kwamba kuwasilishwa Ripoti hiyo kwa lugha ya Kiingereza ni kuikosesha haki ya kuifahamu na kuifuatilia kwa undani Ripoti hiyo, Jee Afisi ya CAG haioni kufanya hivyo ni kuwakosesha wananchi wetu kutambua nini kilichobainika kupitia ukaguzi walioufanya. Jee Afisi ya CAG imekusudia Kamati ya PAC badala ya kufuatilia yale yaliyobainishwa katika Ripoti za Ukaguzi, ifanye kazi ama ya kutafsiri au kutafuta mtaalamu wa kuitafsiri Ripoti hiyo suala ambalo litapoteza muda na kuacha kufanya jambo la msingi kwa mujibu wa Katiba na Kanuni yetu ya Kudumu.

**Mheshimiwa Spika,** ili kulinda matakwa ya Katiba na Kanuni zetu pamoja na maslahi ya wananchi tunaowawakilisha katika muhimili huu, Kamati ya PAC imeipokea Ripoti hiyo lakini haitoweza kuifanyia kazi hadi pale Afisi ya CAG itakapoitafsiri Ripoti hiyo muhimu. Hata hivyo, Kamati yetu inaiomba Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuharakisha utekelezaji wa ushauri wa Kamati yetu ili Kamati iweze kuifanyia kazi ndani ya muda muafaka.

## (B) KUWEPO KWA RIPOTI MPYA ZA UKAGUZI ZILIZOWASILISHWA

**Mheshimiwa Spika,** katika uwasilishwaji huu, Kamati yetu imebaini kwamba Afisi ya CAG imetanua wigo wake wa ukaguzi kwa kufanikiwa kukagua Miradi ya Maendeleo katika ngazi ya Wadi ambayo utekelezwaji wake unasimamiwa na Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa. Kupitia Ripoti hiyo, mambo kadhaa yameibuliwa yakiwemo kuwepo kwa miradi iliyotekelezwa ambayo haikuibuliwa na wananchi, kuwepo kwa miradi iliyotekelezwa chini ya kiwango, kukosekana kwa mikataba ya ujenzi wa miradi ya maendeleo pamoja na kutokuzingatiwa kwa vipaumbele vya maamuzi ya upitishwaji wa Miradi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati za Kusimamia Fedha itafuatilia na kuchunguza na hatimae kutambua ukweli na uhalisia wa mambo yaliyobainika na kuwasilisha ripoti zake hapa Barazani.

**Mheshimiwa Spika,** tunafahamu kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania iliipatia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar jumla ya shilingi bilioni 230.18 ikiwa ni fedha za mikopo za Uviko – 19 zilizoelekezwa katika utekelezaji wa Miradi tofauti ya Maendeleo kwa lengo la kuwarahisishia maisha wananchi wetu.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mara ya kwanza Kamati yetu imebaini kwamba Afisi ya CAG imefanikiwa kukagua na kuwasilisha Ripoti ya Ukaguzi wa Utekelezaji wa Miradi ya Fedha za Mfuko wa Ahueni ya Uviko - 19 Zanzibar kwa Miradi ya Maendeleo katika Sekta ya Afya, Sekta ya Elimu, Sekta ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Sekta ya Nishati na Sekta ya Maji Safi na Salama.

**Mheshimiwa Spika,** Kiujumla, Ripoti hiyo imebainisha uwepo wa dosari lukuki zimejitokeza zinazoashiria uwepo uwezekano wa ubadhirifu na upotevu wa mabilioni ya fedha za Serikali uliotokana na usimamizi na utekelezaji usioridhisha wa Miradi hiyo. Kwa mfano katika sekta ya Afya, kuna jumla ya bilioni 3.28 zimebainika kulipwa kwa Mkandarasi Estim Construction Company ikiwa ni malipo ya ziada yaliyolipwa awali, jumla ya bilioni 4.98 zimetolewa kwa Kampuni ya Group Six International Limited ambayo ilizuiliwa kutoa huduma Zanzibar (blacklisted Companies) kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali za Wilaya ziliopo Kinyasini na Wete na jumla ya shilingi bilioni 48.59 zimefanyiwa manunuzi bila ya kushirikisha Idara husika. Sambamba na hayo, jumla ya shilingi bilioni 20.3 zimedaiwa kutumiwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa ujenzi wa skuli, vyoo na ukarabati wa skuli mbali mbali bila ya maamuzi ya Kamati ya Zabuni na jumla ya shilingi bilioni 8.48 zimetumika kuwalipa Wakandarasi ambao hawakupendekezwa na timu ya tathmini.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu inaahidi kuzichunguza kwa undani dosari zote zilizobainika na kuwasilisha ripoti yake mbele ya Baraza hili ambayo itaweza kubainisha kama kweli kuna upotevu na ubadhirifu wa fedha za umma ama vyenginevyo kwa kutumia njia tofauti za kiuchunguzi.

**Mheshimiwa Spika,** Ripoti hiyo pia imejumuisha Miradi ya Maendeleo iliyotekelezwa kupitia Wafadhili na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikiwemo Miradi iliyotekelezwa kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Wizara ya Ardhi, Maji na Nishati, Wizara ya Kilimo pamoja na Wizara ya Afya.

## (C) KUJIRUDIA KWA DOSARI KADHAA AMBAZO ZILIBAINIKA KATIKA UKAGUZI ULIOPITA

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali inasikitishwa na kushangazwa kwamba pamoja na kubainika dosari kupitia ukaguzi uliopita na juhudi kadhaa kuchukuliwa ili kurekebishwa kwa kasoro hizo. Hata hivyo, bado kuna Taasisi zinaonekana hazioneshi mabadiliko ya matokeo chanya kwani dosari ambazo zimeripotiwa katika Ripoti zilizopita, zimeendelea kujitokeza tena katika Ripoti za Mwaka huu. Kamati imebaini hayo baada ya kupitia Ripoti ya Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Serikali Kuu ambapo dosari zifuatazo zimebainika kujirudia, miongoni mwa dosari hizo ni:

1. Ucheleweshwaji wa kuwasilisha taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka;
2. Kutokuthibitishwa kazini kwa waajiriwa waliomaliza muda wa majaribio (probation priod);
3. Bidhaa ambazo hazikuingizwa katika daftari la ghalani;
4. Kutokukatiwa bima kwa vyombo vya moto;
5. kutokujumuishwa kwa fedha za matumizi katika hesabu za mwisho wa mwaka;
6. Malipo kwa watoa huduma ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma;
7. Malipo ambayo hayakukatwa kodi ya zuio;
8. Matumizi yaliyofanyika nje ya bajeti;
9. Matumizi yaliyofanywa kinyume na vifungu husika;
10. Kukosekana kwa mapato yatokanayo na ukodishwaji wa majengo;
11. Fedha zilizolipwa kwa njia taslim;
12. Kutowasilishwa kwa mapato katika Mfuko Mkuu wa Hazina,
13. Kukosekana kwa hati za malipo;
14. Kuwepo kwa malimbikizo ya madeni tofauti,
15. Kukosekana kwa mikataba ya utoaji wa huduma;

16. Kukosekana kwa hatimiliki za majengo ya Serikali;
17. Kutofikiwa kwa lengo la makusanyo; na
18. Malipo yenye nyaraka pungufu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa msingi huo, Kamati ya PAC ambayo ni moja ya Kamati za Kusimamia Masuala ya Fedha, itazifanyia kazi ipasavyo Ripoti hizi na hatimae kuwasilisha Ripoti yake kwa kina hapa Barazani katika muda muafaka, kama Kanuni za Kudumu za Baraza hili zinavyoelekeza.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kumalizia naomba kuishukuru Ofisi ya Baraza la Wawakilishi kwa ushirikiano mkubwa inayoipatia Kamati yetu wakati wa kutekeleza majukumu yake ukiwemo utekelezaji wa kazi hii ya kuchambua na kutoa maoni ya Kamati juu ya uwasilishwaji wa Ripoti hii ya Ukaguzi. Nawashukuru pia Wajumbe wa Baraza lako Tukufu, kwa kunisikiliza kwa makini na kwa utulivu mkubwa wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha.

……………….
Mhe. Juma Ali Khatib,
**Mwenyekiti,**
**Kamati ya Kudumu ya Kuchunguza na**
**Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC),**
**Baraza la Wawakilishi,**
**Zanzibar.**